TANGAZO LA SERIKALI Na. 28 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO NA MAGULIO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 908 la 2023

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 5

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 5(3) kwa kufuta maneno "Bila kujali" na badala yake kuweka maneno "Bila kuathiri".

Marekebisho ya aya ya 7

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 7(g) kwa kufuta maneno "mkuu wa masoko" na badala yake kuweka maneno "mkuu wa soko".

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu linalohusu FOMU YA KUFIFILISHA KOSA-

(a) kwa kufuta maneno "JEDWALI LA TATU" na badala yake kuweka maneno "JEDWALI LA NNE"; na

(b) kufuta neno "Rorya" katika aya ya pili ya fomu hiyo na badala yake kuweka neno "Mlimba".

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*